Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, kama nilivyosema awali, mbali na mafanikio yaliopatikana, Jumuiya yetu bado inakabiliwa na changamoto kadhaa wa kadha ambazo nyinyi Wabunge wa EALA mnawajibu wa kuzishughulikia. Tuna matatizo ya migogoro; nyinyi ndani ya Afrika Mashariki mnafahamu kwamba kuna maeneo yenye migogoro. Migogoro hii imekuwa ikigharimu maisha ya watu wengi. Changamoto zingine tulizo nazo ndani ya Afrika Mashariki - nataka niwe wazi - ni kuwa, bado vipo vikwazo vya kibiashara, uwekezaji na kutoaminiana ndani kwa wanachama wa East Africa Community. Mara nyingi, huwa hatupendi kuyasema sema haya, lakini mimi nayasema muyabebe ili muijue hiyo *challenges*. - *(Applause)*

Kuna hizo pamoja na changamoto zingine nyingi, nyinyi Wabunge wa Afrika Mashariki, mnatakiwa muanze kuzitoa mapema. Umoja wetu ndani ya nchi za Afrika Mashariki unatakiwa uwe umoja kama tulivyo sisi Marais, Mawaziri, Wabunge, Watendaji wote na baadaye mpaka wananchi wote. - (Applause)

Hivyo, nyinyi kama Wabunge na wawakilishi wa nchi munazo ziongoza, muna jukumu kubwa la kulimaliza. Ifike mahali sisi sote tupendane na tujione ni ndugu. Nafurahi ninapoangalia *arrangement* ya *sitting* mlivyoketi hapa, inaonyesha kweli mmeanza kupendana. Nilitegemea patakuwa *magroup* *magroup* ya watu wa aina fulani wa nchi fulani, lakini mmechanganyika. *This is very good, congratulations.* - (Applause)

Muendeleo hivyo ndugu zangu. Jukumu letu sisi ni kuleta maendeleo ya wananchi wetu tunaowaongoza. Tukianza sisi kuwa na challenges, tutashindwa kuwasaidia wale tunao wawakilisha. Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ya wananchi, si ya viongozi. Pakiwepo na *integration* nzuri miongoni mwa wananchi, Jumuiya hii itadumu milele. Kwa hivyo, *tufacilitate* hili sisi kama viongozi na Wabunge katika kuhakikisha kwamba tunajenga umoja wa wana Afrika Mashariki wa watu wanaoaminiana na kupendana na kujiona kama ndugu.

Mhe. Spika, umesema kuwa umesoma na ulikuwa na Mhe. Kamara shuleni. Wewe inawezekana umeishi Muleba, ukasomea Ihungo Sekondari, ukaenda *form five* shule ya Musoma Sekondari, ukaenda chuo kikuu, University of Dar es Salaam na ulikuwa kiranja katika darasa lako la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. - (Laughter)

Baadaye ulikuwa Director of Public Prosecution (DPP) Rwanda na leo wewe ni

Spika wa EALA. Hii inaonyesha vile sisi wana EAC tunatakiwa kuishi kwa umoja na kupendana kama ndugu. Hili ni muhimu sana, ndio maana nilifurahi uliposema Kiswahili angalau kiendelezwe badala ya kendelea kutumia lugha ambayo ni *thousands and thousands of Kilometres from East Africa*. Tungefurahi kukipiga Kinyarwanda hapa - *mwaramutseho? Namahoro, mulakomeye* au tukapiga Kirundi - *Mwiriwe? Namavuvu urakome, nimuhira barakomeye*, au tukapiga Kiganda - *Mwebale nyo Ssebo, Mwebale nyo Nnyabo*, au Kikenya kijaluo - *Oyaore ngima, wachi madara. Machiga, and so on and so on.* - (Laughter)

Hiyo ndio maana ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, mimi ninawapongeza sana, mnaenda kwa *direction* nzuri na ndio maana mliponialika sikusita kuja. *The past is always history*. Twende mbele kwa manufaa ya EAC. Sambamba na changamoto hizo, zipo zingine mbili ambazo naomba mniruhusu nizielezee kidogo.

Kwanza ni suala la ukosefu wa viwanda. Nchi zetu zina utajiri mkubwa wa rasilimali. Tuna madini. South Sudan ina madini mengi, ina mafuta lakini mabeberu wanataka hiyo nchi iendeleo kukaa ikigombana. Tuna mifugo mingi. Tanzania ni ya pili kwa kuwa na mifugo mingi katika Afrika. Afrika ina bidhaa za kilimo, uvuvi, misitu na kadhalika. Licha ya utajiri huu, ni ukweli usiopingika na kila mmoja wetu anafahamu, kuwa bado hazijatunufaisha vya kutosha. Utajiri huo, hauwasaidii wananchi walio ndani ya EAC zaidi ya watu milioni 170. Moja ya mambo yanayosababisha hali hii nionavyo mimi - kukosekana kwa viwanda vingi kwenye nchi zetu. Matokeo yake, tumekuwa tukiuzia rasilimali zetu nyingi nje ya nchi zetu zikiwa mali ghafi. Hii inatukosesha mapato mengi. Kama mnavyofahamu, bei ya bidhaa ghafi kwa soko la dunia mara nyingi huwa zipo chini.

Mbali na kupoteza mapato, tatizo lingine ambalo mimi naona ni kubwa zaidi ni kwamba, kwa kuuza rasilimali zetu nje ya nchi zikiwa ghafi, maana yake ni kuwa tunazalisha fursa za ajira kwa watu wengine. Tunatengeneza ajira katika mataifa tunayoyauzia mali ghafi zetu. Ni ajira ambazo wananchi wetu wanastahili wazipate. Tungekuwa na viwanda, vingechakata hizo mali ghafi zetu tukazitengeza hapa, watu wetu wangepata ajira na tungeziua zikiwa na thamani kubwa. Hayo ndio maendeleo kwa wananchi tunao wawakilisha. Ni kwa kutambua hilo ndiposa Serikali ninayoiongoza imeweka mkazo mkubwa kwenye suala la ujenzi wa viwanda. Ninafurahi mwikitio umekuwa mkubwa. Wawekezaji wengi wakiwemo kutoka nchi wanachama wa Afrika Mashariki, wanawekeza kwenye sekta ya viwanda hapa nchini. Natumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, mulipe mkazo swala hili la ujenzi wa viwanda. *-(Applause)*

Hususan, kwa kuhakikisha sera na sheria zinazotungwa kwenye Jumuiya yetu pamoja na nchi wanachama, zinawavutia wawekezaji wengi na kulinda viwanda vyetu. Tusipolinda viwanda vyetu, tutakuwa wasindikizaji. Soko la watu milioni 170 ni soko kubwa. Kama tuna mifugo mingi, kwanini tununue viatu kutoka ulaya? Sisi sote tulioko humu pamoja na wewe Mhe. Spika, kiatu chako hicho hakikutengenezewa Afrika Mashariki.

Kwanini? Kwanini tuvae nguo na mashati ambayo yanatokana na pamba lakini tujanunue ya kutoka nje wakati tunazalisha pamba Afrika Mashariki? Haya maswali, sisi kama wawakilishi wa nchi zetu ni lazima tuanze kujiuliza. Kwanini tununue nyama kutoka nje wakati tuna mifugo inazunguka hapa na saa nyingine inakosa biashara? Kwanini tununue samaki wakati ukitoka

huku chini mpaka kwenye mpaka karibu na Somalia ni bahari kubwa? Ziwa Victoria limezunguka nchi nne. Tuna mito kila mahali, kwanini tumeshindwa kuvua samaki tuwauze humu na kwenye soko lingine? Sasa tunaletewa samaki ambao ni *low quality*. Haya maswali ni lazima tujiulize. Ni maswali mengi sisi kama Wabunge - Mhe. Spika *I just want to be open* - tukijiuliza vizuri, tutasaidia *kutransform* wananchi wetu na Bunge hili likawa Bunge lenye historia katika maendeleo ya Afrika Mashariki.

Ninajua katika kufanya haya, mtakutana na *challenges* nyingi. Wenzetu wengi ambao si wanachama wa EAC wangependa kulitumia hili eneo la EAC katika soko lao. Hatuwazuii, lakini twende *on a win-win situation*.

Tumetumika mno, ni lazima tufike mahali tuanze kujua mahali tuliko toka, mahali tulipo na mahali tunapoelekea kwa manufaa ya wananchi wetu ambao wengi wao ni maskini.

Changamoto ya pili Mhe. Spika na waheshimiwa Wabunge ambayo nayo ningependa nielezee kidogo, ni kipaumbele cha pekee kuhusu ujenzi na miundombinu hususan, usafiri na nishati ya umeme. Miundombinu hii ni muhimu sana katika kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi miongoni mwa mataifa. Hata swala la kukuza viwanda haliwezi kufanikiwa endapo nchi yetu itashindwa kuboresha na kuimarisha miundombinu hii. Pamoja na ukweli huo, ni bahati mbaya tafiti zilizofanyika miaka kadhaa ya nyuma zilionyesha kuwa ukanda wetu wa Afrika unakabiliwa sana na matatizo ya miundombinu ya usafiri na nishati ya umeme. Hii imefanya gharama za usafiri na umeme kuwa juu sana. Mathalani, tafiti zinaonyesha kuwa gharama za usafiri kwenye ukanda wetu ni mara nne hadi mara tano ukilinganisha na nchi za Asia Mashariki, Marekani na Ulaya na zinachangia

kuongezeka kwa gharama za bidhaa kwa asilimia arobaini.

Kutokana na tatizo la usafiri na umeme, bidhaa zetu tunazozalisha hapa gharama zake itakuwa mara arobaini zaidi ukilinganisha na bidhaa zinazozalishwa mahali pengine. Umeme pia umeonekana kuwa si mwingi. Mathalani, kwa mujibu wa taasisi ya Power Africa mwaka wa 2015, nchi zote sita, wanachama wa Afrika Mashariki, ukijumlisha na Sudan Kusini, zilikuwa na takriban megawatts 6,500 tu. Nadhani, si lazima mtu awe mtaalamu wa hesabu au uchumi ili aweze kufahamu kuwa kiwango hiki cha umeme ni kidogo kuweza kuhimili mahitaji ya uchumi wa kisasa - megawatts 6,500. Kenya ndio kidogo, wana megawatts nyingi. Sisi Tanzania tuna 1,500 megawatts tu. Nazifahamu za Uganda, Burundi, Rwanda na South Sudan na nyinyi mnazifahamu. Ukiwa na megawatts 6,500 tu, kujenga viwanda ni challenge kubwa. Ndio maana bei ya umeme ndani ya Afrika Mashariki ipo juu sana ukilinganisha na bei ya umeme kwenye nchi zenye viwanda. Mara nyingi, tumekuwa tukikumbatia wawekezaji ambao baadaye tunawalipa *capacity charges*, kisha wao ndio wanaofaidika badala ya kuwasaidia wananchi wetu na viwanda vyetu. Hili nalo ni *challenge* kubwa.

Kwa hivyo, waheshimiwa Wabunge mkiongozwa na Mhe. Spika, hili nalo mnatakiwa kuliweka maanani, ni namna gani changamoto hii tunaweza kupambana nayo ndani ya Afrika Mashariki. Tuna vyanzo vingi, lakini inawezekana hatuvitumii. Pamoja na changamoto zilizopo, ni ukweli usiopingika kuwa katika miaka ya hivi karibuni, nchi wanachama zimejitahidi sana kuimarisha miundombinu. Kwa mfano, katika barabara, hivi sasa mtu anaweza kutoka Dodoma kwenda Kampala, Kigali na Nairobi kwa barabara ya lami. Hivi ni vitu ambavyo siku za nyuma vilikuwa haviwezekani. Barabara nyingi zinaendelea

kujengwa na Mhe. Spika umelizungumza. Kwa mfano, sisi Tanzania tunaendelea na ujenzi wa barabara ya kuiunganisha mikoa ya Tabora na Kigoma jumla ya kilomita 359 kutoka Tabora kuenda Mpanda na maeneo mengine. Pia, tunaendelea kuunganisha katika maeneo mengine ya Burundi na Rwanda kama ulivyozungumza, Mhe. Spika. Aidha, tunajenga barabara ya Nyakanazi hadi kidawe ambayo itaboresha usafiri kati ya wenzetu pamoja na Uganda. Mifano ni mingi.

Kando na barabara, hivi sasa ndani ya Jumuiya yetu, kuna miradi mingi mikubwa ya miundombinu ya usafiri inayotekelezwa na baadhi yao kwa ushirikiano wa nchi wananchama. Mathalani, ndugu zetu wa Kenya tayari wamekamilisha ujenzi wa reli ya kisasa kutoka bandari ya Mombasa kwenda Nairobi ambayo inalenga kuboresha usafiri kwenye ushorobo wa kaskazini yaani Northern Corridor. - (*Applause*)

Sisi Tanzania, tumeanza kutekeleza mradi wa kupanua bandari ya Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa - *Standard Gauge*, ili kuboresha usafiri kwenye ushorobo wa kati yaani *Central Corridor* ambao utahudumia nchi za Burundi kwa kuunganishwa sehemu ya Uvinza na Msongati na Rwanda kwa kuunganisha sehemu ya Isaka, Rusumo hadi Kigali na Uganda pia na nchi ya Democratic Republic of Congo (DRC).

Tunakarabati meli zetu na tumeanza kujenga meli mpya kubwa kwa ajili ya kuboresha usafiri kwenye Ziwa Victoria. Kama mnavyofahamu, ziwa hili ni kiungo muhimu cha usafiri kwenye Jumuiya yetu, hususani, kwenye nchi zinazounganisha ziwa hilo, yaani Tanzania, Kenya na Uganda. Inakadiriwa kuwa takriban watu milioni 40 wanaishi karibu na ziwa hili.

Ninacho waomba, Mhe. Spika na Bunge la Afrika Mashariki, tujiamini katika kutekeleza miradi, tusifikiri kila mradi lazima upate *support* ya wafadhili kutoka nje. *Never!* Wale saa nyingine wana masharti yao na masharti yao saa nyingine yanaendana na *feasibility study* na *detailed design, update design consultant and so on*. Unakuta gharama unazotumia ni mara kumi zaidi ya gharama kama ungejibana wewe kama nchi. Ninalizungumza hili si kwa sababu hatuhitaji misaada na ushirikiano, ni lazima hili tulitilie maanani. Tukiamua tunaweza. Mifano ipo, ni mingi. Sisi wenzenu, Tanzania tumejaribu tukaona tunafanikiwa. Ndio maana tumeweza kujenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma kilomita 700.26 kwa thamani ya trilioni 7.6 *Tanzanian Shillings*. Hatujapata mkopo au senti zozote kutoka nje na *cost* imekuwa chini. Tumeweza kununua ndege sita na hatukuomba mkopo. Tunajenga meli kubwa kwenye Ziwa Victoria na hatukuomba mkopo na mengine mengi. - (*Applause*)

Tukiamua kuwa *conciatise* wananchi wetu, nina uhakika – na utajiri tulio nao ndani ya Afrika Mashariki - tutashirikiana kwa pamoja. *Experience* ya Tanzania tuipeleke Rwanda na ya Rwanda tuipeleke Burundi, ya Burundi tuipeleke Uganda na ya Uganda tuipeleke Kenya, ya Kenya tuipeleke South Sudan tutajiona kama ndugu wa kweli, sio ndugu juu juu wa kuangaliana angaliana. *It is supposed to come from the blood and the heart, to cement it inside* kwa lugha mlioizoea. Nataka kuwahakikishia Mhe. Spika, we shall make it. Tutafanikiwa kisawasawa. - (*Applause*)

Ndugu zangu, kwenye miundombinu ya usafiri, pia tunashirikiana na wenzetu wa Uganda kutekeleza mradi mkubwa wa bomba la kusafirisha mafuta yaani la, East Africa Oil Pipeline kutoka Hoima hadi bandari ya

Tanga pamoja na miradi mingine mingi. Kuhusu nishati ya umeme, kama mnavyofahamu, nchi yetu imegundua kiasi kikubwa cha gesi, takriban tani za ujazo trilioni 57. Ipo gesi; lakini si gesi tu ya *Ethyl*, tumegundua pia kuna gesi ya *Helium* ambayo inapatikana katika nchi tatu tu duniani. Ipo! Hivi haviwezi kuwanufaisha Watanzania tu, gesi hizi zinatakiwa ziwanufaishe wana East Africa wote. - (*Applause*)

Pia, tumeanza kutekeleza miradi mingi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi hiyo na tupo mbioni pia kuanza ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme kwa kutumia maji yaani Stieglers Gorge. Mradi huu uliobuniwa na baba wa taifa hili, Mwalimu Julius Kabarage Nyerere na tukauacha kwa muda mrefu, utakuwa *solution* ya tatizo la umeme katika nchi hii kwa sababu utatoa megawatts 2,100.

Tunataka kwanza tuwe na umeme mwingi ambao, kwa pamoja, umeme huo tutaweza kuwauzia kwa bei ya chini ndugu zetu walioko ndani ya EAC. Pili, tumelenga kupunguza uzalishaji wa umeme wa mafuta ili kuifanya bei ya umeme nayo iwe chini. Sambamba na hilo, tunashirikiana na nchi zingine wanachama kutekeleza baadhi ya miradi. Tunatekeleza mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilowatts 400 na wenzetu wa Kenya unoanzia Zambia kupitia hapa Tanzania na kuelekea Kenya. Tunatekeleza na Uganda mradi wa kufua umeme wa Kikagati Mlongo. Aidha, tuko kwenye majadiliano na Rwanda pamoja na Uganda kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme pale Songezi. Nchi zetu lazima ziende pamoja. - (*Applause*)

Ni imani yangu kuwa miradi hii pamoja na ile inayotekelezwa kwenye nchi zingine wanachama, yote itakapo kamilika, tutakuwa

tumefikia kuimarisha huduma za usafiri na upatikanaji wa umeme kwenye nchi zetu. Hilo likitokea, hatutakuza sekta ya viwanda tu, bali pia ushirikiano wetu na kasi ya ukuaji wa uchumi kwenye Jumuiya yetu utaongezeka. Hivyo basi, nawasihi Wabunge wa Afrika Mashariki mlipе kipaumbele cha kipekee suala hili la ujenzi wa miundombinu. Kama mnavyofahamu, ujenzi wa miundombinu una gharama kubwa, lakini tukishirikiana kwa pamoja na tuka *share experience* miongoni mwetu tukishirikiana na wenzetu pia wa nchi zingine, nina uhakika tunaweza tukafika mahali pa kulikomboa taifa hili na mataifa yetu haya. Mungu ametupa Afrika Mashariki yenye utajiri mkubwa, lakini utajiri huu hatuutumii. Saa nyingine tunagogeshwa na mabeberu ili tuchelewe kuutumia vizuri utajiri wetu. Tunaingia kwenye mambo ambayo ni *too parochial* badala ya *kuconcentrate* kwa mambo ambayo yatawahudumia wananchi wetu kwa ajili ya manufaa ya wana EAC.

Nyinyi Waheshimiwa Wabunge, mnayo nafasi ya kuwashawishi wananchi wetu na wawekezaji kutoka nje. Nimefurahi kuona Waheshimiwa Mabalozі wako hapa pamoja na *development partners* wengine ambao nina uhakika watazishawishi nchi zao ziendelee kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki katika kuleta maendeleo ya kweli ya wananchi waliomo ndani ya nchi hizi. Kwa hivyo, tukishirikiana nao on the *win-win situation*, tutaweza kulijenga vizuri na kuendeleza wananchi wetu ambao kwa kweli wana umaskini mkumbwa. Maskini wa Tanzania hawana tofauti na maskini wa Burundi, hawana tofauti na maskini wa Rwanda, hawana tofauti na maskini wa Uganda, hawana tofauti na maskini wa Sudan Sudan na hawana tofauti na maskini wa Kenya. Watu wetu ni maskini; sisi kama viongozi ambao tumechaguliwa kwa niaba ya wananchi maskini ni lazima *tusacrifice* kwa ajili ya maendeleo yao. - (Applause)

Ndio maana nimeendele kuisisitiza, masuala ya ushirikiano, umoja na kutokubaguana. Hilo ni jambo muhimu sana. Suala la kupendana ni lazima liwe muhimu sana, suala la tofauti zetu ndogo ndogo lazima tuliondoe haraka sana. Tukifanya haya yote, tutafanikiwa na watu walioko ndani ya Afrika Mashariki watawaheshimu kwa kuwa Wabunge wa Bunge la Nne la Afrika Mashariki ambalo ni Bunge kwa ajili ya watu wanyonge.

Katika hili - si kwamba linahusika hapa sana, lakini kwa sababu Secretary General wa EAC yuko hapa, washughulikie miradi inayoanzishwa kwa *speed* kubwa. Pamekuwa na *speed* ndogo katika kushughulikia miradi hii. Najua kwa mfano, mradi wa Malindi, Horohoro hadi Bagamoyo sasa ni zaidi ya miaka kadhaa. *Feasibility study* na *detailed design* zimeshamalizika na sijamuona *contractor* na miradi mingine mingi. Sitaki niitoe hapa, lakini nimeona nichomekee hapa ili na yeye aondoke na *message* atakapo ondoka hapa. - (Laughter)

Waheshimiwa Maspika na Waheshimiwa Wabunge, ningependa pia kutumia fursa hii kuwahakikishi Wabunge wa Afrika Mashariki kwamba sisi Tanzania tutaendelea kushirikiana na nchi zote pamoja na wanachama wote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutimiza dira na malengo ya jumuiya hii. Nataka niwahakikishie, Tanzania iko pamoja na nyinyi. - (Applause)

Yale maamuzi mengine yanayo chelewa chelewa, nataka kuwahakikishia tutayapeleka *speed* kweli kweli ili yale maamuzi yawe na maslahi mapana katika Afrika Mashariki. Tusipelekeshe na wengine. Ni lazima katika maamuzi yote tuwe tunafanya *evaluation* ya kutosha hasa katika mikataba tunayo ingia na wengine ambayo si miongoni mwa EAC. Katika hili,

ningependa kuwaarifu kuwa mwaka jana nchi yeti iliridhia itifaki ya Jumuiya kuhusu maswala ya amani na usalama yaani Protocol on Peace and Security. Mapema mwaka huu, nchi yetu ilizindua *passport* mpya ya kielekitroniki ya Afrika Mashariki na ya Tanzania kama ilivyo amuliwa na Jumuiya yetu. - (Applause)

Hii yote ni kudhibitisha kuwa Tanzania inaheshimu maamuzi ya Jumuiya hii. Jumuiya yetu inazidi kukuwa na hivi sasa ina wanachama zaidi ya milioni 170. Hii imeiongezea nguvu na kama tutaendelea kushirikiana, nina imani Jumuiya yetu itazidi kuimarika na sauti yake itaongezeka na tutaheshimika kimataifa. Ninyi Wabunge wa Afrika Mashariki ni kiungo muhimu katika kuhakikisha hili linafanikiwa. Mukiwa wawakilishi wa wananchi mnayo nafasi kubwa ya kuwaunganisha wana Afrika Mashariki wote pia, kuwaelimisha na kuwatahadharisha dhidi ya watu wenye nia mbaya ya Jumuiya yetu. Ni wajibu wenu kuwaelimisha wananchi ili umoja na mshikamano uzidi kudumu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Baba wa taifa letu, mmoja wa waasisi wa Jumuiya hii, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema, nikimnukuu kwa lugha ya Kiiingereza: *"Unity will not make us rich, but it can make it difficult for Africa and the African people to be disintegrated and to be disregarded and humiliated."* Mwisho wa nukuu.

Kwa ujumla, nchi yetu inaendelea vizuri. Kama mnavyofahamu, uchumi wa nchi yetu ya Tanzania unakuwa kwa asilimia 6.8 hadi asilimia 7 na *inflation* iko asilimia nne. Muungano wetu unaendelea vizuri na Tanzania tuna *experience* ya kuungana. - (Applause)

Kesho kutwa, Muungano wetu utafikisha miaka 54. Mhe. Spika kwa sababu bado mpo hapa Dodoma, na Mheshimiwa Mkuu wa

Mkoa bado yupo hapa, ninawakaribisha Wabunge kwenye siku hiyo ya muungano hapa Dodoma.

Mhe. Spika, waheshimiwa wabunge na ndugu viongozi, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru Wabunge wa Afrika Mashariki kwa kunialika kulihutubia Bunge lao. Narudia tena, Serikali ninayoiongoza itatoa ushirikiano wa kutosha kwa Bunge hili.

Namshukuru pia Mhe. Spika pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Ndugai kwa kuridhia shughuli hii ifanyike hapa kwenye eneo lenu. Hili linadhihirisha uhusiano mzuri uliopo kati ya Bunge hili na Bunge la Afrika Mashariki pamoja na Wabunge wanachama. - (Applause)

Ningependa pia kutumia fursa hii kushukuru na kupongeza vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Dr. Bilinith Mahenge kwa kuwapokea vizuri wageni wetu na kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea. Asanteni sana. Nawashukuru pia wananchi wa Dodoma kwa jumla kwa kuendelea kuwapokea wageni wetu.

Mhe. Spika na Wabunge Waheshimiwa, nilifundishwa na Mbunge wa hapa Dodoma kuwa wanasiasa huwa tuna mwisho na mwisho kabisa. Sasa naomba niseme la mwisho kabisa. - (Applause)

Hapa naomba ninukuu maneno mengine ya Mwalimu Nyerere aliyoyasema kwenye sherehe ya miaka 50 za uhuru wa Ghana. Nanukuu: *"Kizazi changu, kiliongoza jitihada za kuleta uhuru wa kisiasa wa bara letu. Kizazi cha sasa cha waafrika hakina budi kuchukua kijiti pale tulipoachia na kwa nguvu mpya kusukuma mbele maendeleo ya bara letu."* Mwisho wa nukuu. - (Applause)

Kwa kutumia maneno hayo ya Mwalimu Nyerere, ningependa nitoe wito kwenu nyinyi waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na wana Afrika Mashariki wote, kushikamamana, kushirikiana, na kwa pamoja tushike kijiti na kuendeleza pale walipoishia waasisi na viongozi wetu waliotangulia.

Mungu libariki Bunge la Nne la Afrika Mashariki, Mungu ibariki Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Asanteni sana kwa kunisikiliza. Nawashukuru sana. - *(Applause)*

The Speaker: Mhe. Rais, tunashukuru sana kwa mawaidha. Tutaondoka hapa na nguvu mpya na ari mpya, We will not be the same when we leave this place.

Hon. Members, when I introduced the visitors I did not introduce the Members because they are not visitors. However, I have to, with your permission; I will do that by Chapters. Before that, I will introduce one Council Member who is ever present in our sittings. Dr. Susan Kolimba.

You will appreciate the fact that she is one of the Council Members who are always present whenever we have a sitting.

Mhe. Rais, naomba niwatambulishe Wabunge *chapter by chapter*. Nianze na waheshimiwa Wabunge from the Republic of Burundi (*honourable Members from the Republic of Burundi stood up in their places for recognition*), from the Republic of Kenya (*honourable Members from the Republic Kenya stood up in their places for recognition*), from the United Republic of Tanzania (*honourable Members from the United Republic of Tanzania stood up in their*

places for recognition), from the Republic of Rwanda (*honourable Members from the Republic of Rwanda stood up in their places for recognition*), from the Republic of Uganda (*honourable Members from the Republic of Uganda stood up in their places for recognition*) and from the Republic of South Sudan (*honourable Members from the Republic of South Sudan stood up in their places for recognition*). - *(Applause)*

Your Excellency, I had permission to do everything but one function which honourable Members decided to delegate to another Member. Wanajua kwamba wewe una imani na vijana na katika uongozi wako, umewapa vijana wengi majukumu makubwa. Mhe. Rais husemi kwamba vijana ni viongozi wa kesho, unajua kuwa ni viongozi wa leo.

Sasa, Hon. Members have chosen one young member to be the one to move the vote of thanks. Hon. Dennis Namara from Uganda. - *(Applause)*

VOTE OF THANKS

Mr Dennis Namara (Uganda): Your Excellency, Dr. John Pombe Joseph Magufuli, President of the United Republic of Tanzania; Rt. Hon. Martin Ngoga, Speaker EALA; Rt. Hon. Majaliwa Kassim Majaliwa, Prime Minister of the United Republic of Tanzania; Rt. Hon. Job Ndugai, the Speaker of the National Assembly of Tanzania; Rt. Hon. Kirunda Kivejinja, Chairperson Council of Ministers and all the Hon. Members of the Council of Ministers present; the Rt. Hon Amb Liberat Mfumukeko, the EAC Secretary General; Honourable Members of EALA; and Hon. Members of the National Assembly; Your Excellencies Ambassadors and all protocols observed.

Your Excellency, I would like to take this opportunity to say that I am extremely delighted to have been given this very rare

chance to move a vote of thanks on behalf of my colleagues, the Members of EALA. I want to thank you, first of all, for accepting to come and address the Fourth Assembly and also for your precise, concise and extremely insightful information regarding the East African integration. - *(Applause)*

Your Excellency, I must say that we are extremely grateful. As one person said – and I believe it today – some men are born great, others achieve greatness and others collide with greatness. Your Excellency, indeed, you were born great and you have achieved greatness. - *(Applause)*

Your Excellency, you have, indeed, diagnosed the problems of East Africa and Africa in general and shown us what we need to do as Members of EALA to find lasting solutions to the challenges facing our people. Also, you have told us and, indeed, appreciated the role that we are playing as EALA and EAC as far as implementing the programmes the policies and protocols that have been initiated by the Summit of the Heads of State. Your Excellency, as you have said, since we came to Dodoma – we appreciate that we came to Dodoma – it goes without saying that the people of Dodoma are extremely hospitable. - *(Applause)*

I want to thank you for allowing us to be here. We came here and we have been able to go through some of the important Bills that will spur the EAC to another level. First, we have touched on the third pillar of integration through the Monetary Institute Bill that went through here in Dodoma. We are also moving forward to ensure that the pace at which we would want this Bill to become law and be implemented is what we will concentrate on.

Your Excellency, in particular, we want to thank you for your outstanding commitment

towards the East Africa integration. You are one of the Heads of State that has not missed any Summit of the Heads of State. - *(Applause)*

That shows the zeal, charisma and commitment that you have towards the East Africa integration. We want to thank you, Mr. President.

Your Excellency, The United Republic of Tanzania has fulfilled its financial obligations 100 per cent to the EAC. - *(Applause)*

Your Excellency, we cannot take that for granted. We are extremely grateful and we now see that, indeed, you are committed towards the East Africa integration.

Your Excellency, as we move forward, you have talked about the challenges that face East Africa and you have also provided some solutions. We thank you together with the other Heads of State in EAC for having initiated some of the infrastructural projects that will go a long way to spur industrialisation of the people of East Africa and, therefore solve the socio economic challenges that we all face. First, the crude oil pipeline, starting all the way from where I come from Hoima - that is my region - up to Tanga. - *(Applause)*

Your Excellency, we are grateful and we know this will go a long way in solving some of the challenges. You have talked about Industrialisation. We cannot move this economy of East Africa forward unless we industrialise. You have talked about the big market, the 170 million people that we have with a big combined GDP of 150 million dollars. Why do we not harness that to spur our East African economy to greater horizons?

Your Excellency, as the Fourth EALA, we will fast track the programmes and projects that are supposed to be implemented by EAC with your support.

Your Excellency, your commitment towards young people is impeccable. This is seen in the Members you sent to EALA, they are youthful. As a young person, I have also had an opportunity of knowing some of the deep challenges that face our people. I have realised that it is not about age neither is it about biology. It is about ideology, how one thinks and their maturity. The people you sent from the United Republic of Tanzania to EALA, the young Members, are doing a tremendous job. Thank you.

Your Excellency, my work was just to move a vote of thanks. I will not divulge into other work that is not mine, but I would want to thank you, on behalf of all the Members here. We are looking forward to be visiting other cities in Tanzania because the generosity and hospitality of the people of Tanzania is beyond horizons. - (Applause)

Thank you, your Excellency, may God bless you.

Ahsanteni sana, Mungu akubariki.

The Speaker: Thank you, Hon. Dennis Namara for speaking our minds eloquently. That is what each one of us would have wanted to say. However, we had to choose one of us to represent us.

Hon. Members and our guests, I want to thank you for honouring us with your time.

ANNOUNCEMENT

Before I adjourn, I want to make a few announcements. There will be a group photograph and the protocol team will lead us in that process. After that, we shall share a cup of tea in the Parliamentary Canteen. I think all of you have had time to visit the canteen.

ADJOURNMENT

On that note, I now adjourn the House until tomorrow Wednesday, 25th April 2018 at 2.30. Thank you.

*(The House rose at 4.10 p.m. to
reconvene on Wednesday,*

25th April at 2.30 p.m.)